THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TANZANIA AGRICULTURAL RESEARCH INSTITUTE

TARI

TARI Mikocheni, Mikocheni B, Plot 22 Along the Coca Cola Road,
P.O. Box 6226,
Dar es Salaam.
Telephone No: +255 222 700 552
Email: cmmikocheni@tari.go.tz

# MAFANIKIO TARI MIKOCHENI



Waziri wa Kilimo
Hussein Bashe



Katibu Mkuu Wizara ya
Kilimo Andrew Massawe



Mkurugenzi Mkuu wa TARI
Dkt. Godfrey Mkamilo



Meneja wa TARI Mikocheni
Dkt. Joseph Ndunguru



Aina mbalimbali za miche ya muhogo zikiwa kwenye maabara ya Mikocheni iliyotokana na uzalishaji kwa kutumia teknolojia ya (tissue culture) uzalishaji miche kwa njia ya chupa.



## Utafiti wa TARI Mikocheni unavyoinua zao la Minazi

Na BARAKA LOSHILAA

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 10 ya mwaka 2016, ikiwa na majukumu ya kutafiti, kusimamia, kuratibu na kuhamasisha utafiti wa kilimo nchini.

Dhima ya Taasisi hii, ni kugundua na kuhimiza matumizi ya teknolojia mbalimbali za kilimo, ili kuongeza tija, uhakika wa chakula, lishe pamoja na kuwa na kilimo endelevu chenye kuharakisha ukuaji wa uchumi nchini.

Taasisi hii ina mtandao wa vituo 17 vya utafiti, mojawapo ikiwa ni TARI Mikocheni, ambacho kimepewa majukumu ya kuendeleza utafiti wa zao la inazi, mazao miti kwa upande wa Pwani, machungwa, miembe na korosho pamoja na kufanya utafiti wa kuhusisha mifumo ya biolojia kuzalisha bidhaa na kuboresha sekta ya kilimo.

**UTAFITI WA MINAZI**

Meneja wa Kituo cha TARI Mikocheni Dkt. Joseph Ndunguru anaanza kwa kueleza kwamba minazi ni muhimu kwani ni zao la kilimo mseto kwa wakulima wadogo katika nchi yetu ya Tanzania. Zao hili linalimwa kwa wingi kwenye ukubwa wa 265,000 ha katika ukanda wa Pwani ya Tanzania Bara na Visiwa vya Zanzibar. Maeneo mengine yanayolimwa zao la minazi ni pamoja na mikoa ya Kigoma, Wilaya ya Kyela-Mbeya, Mwanza katika fukwe za Ziwa Viktoria. Zao hili linastawi vizuri katika maeneo yenye hali ya hewa yenye kiasi cha nyuzi joto la 27, zaidi ya 2000mm za mvua zilizo na mgawanyiko mzuri, zaidi ya asilimia 75 ya unyevunyevu, jua la kutosha na kwenye udongo unaopitisha maji kwa urahisi.

Takwimu za kilimo cha minazi nchini kwa mwaka ni tani 546,301 na utafiti uliofanywa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni ambacho kina jukumu la kusimamia maendeleo ya zao la minazi kitaifa ulibaini kwamba mti mmoja wa minazi unakadiriwa kuwa na mavuno ya kiasi cha nazi 35-45 kwa mwaka. Kupitia utafiti wanaofanya Dkt.Ndunguru anaeleza kuwa, wanalenga mti mmoja wa minazi kuzalisha nazi 70 kutoka nazi 45.

Dkt. Ndunguru anaendelea kwa kueleza kwamba zao la minazi lina umuhimu mkubwa ndani na nje ya nchi yetu kwani:

- Huchangia katika pato la Taifa kwa asilimia
- Hutumika kama chakula
- Hutumika kama mali ghafi katika viwanda kwa kuzalishia mafuta, mbao na samani zake n.k
- Huliingizia Taifa fedha za kigeni

Dkt.Ndunguru anasema wanafanya utafiti wa minazi, kuzalisha mbegu, kuzisambaza kwa wakulima na kufundisha uongezaji wa thamani.



Zao la mnazi

"Tunazalisha mafuta mwali yanayotokana na nazi. Mafuta haya yana manufaa mengi kiafya na sasa yana soko kubwa sana nchini. Ili kuongeza teknolojia ya uongezaji thamani wa zao la minazi, tumefundisha wakulima na wadau mbali mbali kwa sasa wanazalisha mafuta haya kwa kushirikiana na kituo chetu.

Dkt.Ndunguru anasema, minazi huathiriwa na ugonjwa wa kunyong'onyea na wadudu aina ya chonga, hivyo wana mbinu shirikishi kudhibiti wadudu hao.

Inaendelea...

# Ongezeko uzalishaji wa Muhogo, mafanikio TARI Mikocheni

Akizungumzia zao la muhogo Dkt.Ndunguru anasema, muhogo ni zao la biashara na chakula na hulisaidia taifa wakati wa ukame, hivyo humuhakikishia mkulima chakula.

Kuhusu mafunzo ya mbinu bora za kilimo Dkt.Ndunguru anasema, wanawafundisha wakulima matumizi bora ya viuatilifu, kilimo bora cha minazi na mihogo.

Dkt.Ndunguru anaeleza kuwa, wamefanya utafiti kudhibiti magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia ambayo hushambulia zaidi mihogo.

Anabainisha kuwa maeneo ambayo wakulima walikuwa wakipata mazao chini ya tani nane, baada ya kupatikana mbegu zilizofanyiwa utafiti na TARI Mikocheni, uzalishaji umeongezeka kufikia tani 35 hadi 40, hatua ambayo imeongeza kipato cha wakulima na kuongeza hali ya chakula.

"Tumesambaza mbegu za mihogo katika mikoa ya Tanga, Kanda ya Ziwa, Mara, na mikoa ya Kusini. Katika wilaya ya Mbinga kulikuwa na vikundi vya wakulima 51 na katika usambazaji tumekuwa tukivitumia vikundi hivyo vya wakulima," anaeleza.

Akizungumzia mbegu za mihogo Dkt. Ndunguru anasema, zimegawanyika katika kanda ikiwemo Pwani ambayo hujumuisha mbegu za Kiroba ambazo zilifanyiwa utafiti na katika uzalishaji hutoa mazao mengi ambapo "Mkulima hupata tani 35 hadi 40 badala ya tani 8". Kuna mbegu za ukanda wa kati ambazo hustahimili ukame kama Hombolo na Mumba; zinazofaa kwa Nyanda za Juu na Ukanda wa Ziwa ni Mkombozi na hizi huzaa sana, Nyanda za Kusini kuna Naliendele, Kibaha ni aina za mbegu ambazo huzaa sana

Hivyo mkulima akitaka mbegu tunamshauri tujue yuko wapi ili apewe mbegu kulingana na eneo lake,"anabainisha.



Utoaji wa mafunzo kwa watafiti wachanga ili kuwajengea uwezo wa kutambua magonjwa ya mazao

> **Tumesambaza mbegu za mihogo katika mikoa ya Tanga, Kanda ya Ziwa, Mara na mikoa ya Kusini. Katika wilaya ya Mbinga kulikuwa na vikundi vya wakulima 51 na katika usambazaji tumekuwa tukivitumia vikundi hivyo vya wakulima.**
>
> **Dkt. Ndunguru**

**VIJANA NA KILIMO**

Dkt. Ndunguru akizungumzia uwezeshwaji wa vijana katika kilimo, anasema, TARI Mikocheni inapenda vijana kujikita katika kilimo hivyo ili kuwavutia lazima kuwe na kilimo chenye tija na cha biashara.

"Tumeshatoa mafunzo kwa vikundi vya vijana katika wilaya ya Bagamoyo, mikoa ya Morogoro na Iringa kufundisha vijana namna ya kuzalisha miche ya mbogamboga, kama pilipili hoho na nyanya," anaeleza.

Anasema vijana hao huuza miche kwa wadau na kujipatia fedha hatua ambayo anaielezea kuwavutia vijana wengi.

**UCHUMI WA KIDIPLOMASIA**

Dk.Ndunguru anasema wanatekeleza miradi mingi ya kimataifa kwa kushirikiana na nchi mbalimbali.

"Tulikuwa na mradi wa uboreshaji zao la muhogo ambao ulikuwa ukitekelezwa katika nchi saba ambazo ni Tanzania, Kenya, Rwanda, Msumbiji, Uganda, Zambia na Malawi hivyo kupitia mradi huu maabara zimejengwa na kutolewa mafunzo kwa wataalamu, hivyo tunahakikisha mbegu ambazo hazina magonjwa wakulima wanatumia kuongeza tija," anaeleza.

Pia anabainisha kuwa, teknolojia ambazo zimegunduliwa na watafiti huuzwa kwa makampuni. "Tunapozalisha miche bora ya migomba, hizo teknolojia tunauza kwa sekta binafsi kwa wingi zaidi ili kuwafikia watu wengi zaidi na ili kufanya zoezi hili kwa ufanisi tuna kitengo cha kubiasharisha teknolojia zetu," anaeleza.



Mtafiti Christina Kidulile akionesha namna wanavyozalisha mbegu kupitia teknolojia ya chupa



Dkt. Tairo akifanya utafiti katika moja ya maabara ya TARI Mikocheni